



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: 0232935443  
Nukushi: 0232935442  
Baruapepe.td@nanyambatc.go.tz

2 Barabara ya Bomani,  
S.L.P 1490,  
63682 NANYAMBA-MTWARA

Kumb. Na. NTCC/R.60/8/09

Tarehe 29/09/2023

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Mji Nanyamba imepata kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb. Na.FA.170/360201B/101 cha Tarehe 05 Septemba,2023 kwa ajili ya kuajiri Dereva Daraja la II –Nafasi moja (1) na Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II –Nafasi moja (1).

Hivyo, Mkurugenzi wa Mji Nanyamba anawatangazia watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Mji Nanyamba, kuomba nafasi za kazi za Dereva Daraja la II na Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II kuanzia leo tarehe 29/09/2023.

### 2.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II - TGS C (Nafasi 1)

#### 2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu Mafunzo ya Stashahada au NTA Level 6 katika moja ya Fani zifuatazo:

Utunzaji wa Kumbukumbu, Urasimu Ramani (Cartography) au Geoinformatics, Sheria au kumbukumbu za Afya kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali. Pia awe na Ujuzi wa Kompyuta

#### 2.2 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara ni TGS C1.

### 2.3 KAZI/ MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II

- i. Kuorodhesha barua zinazolingia Masijala kwenye Rejista.
- ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi kwenye Rejista.
- iii. Kusambaza majalada kwa watendaji (Action Officer)
- iv. Kupokea majalada yanayorudi Masijala toka kwa Watendaji
- v. Kutafuta majalada/ nyaraka/kumbukumbu zinazohitajika na watendaji
- vi. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada au mahali pengine yanapohifadhiwa
- vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi
- viii. Pamoja na kazi zingine utakazopangiwa na Mwajiri wako.

### 3.0 DEREVA DARAJA LA II - TGS B (Nafasi 1)

#### 3.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji wa Magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha Ajali.

Awe amehudhuria Mafunzo ya msingi ya uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au NIT au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 3.2 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara ni TGS B1.

### 3.3 KAZI/ MAJUKUMU YA DEREVA DARAJA LA II

- i. Kukagua Gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa Gari
- ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya Gari
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- vi. Kufanya usafi wa Gari
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake wa kazi

### 4.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu.
- iv. Maombi yote yaambatane na picha 2 (passport size), nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, nakala ya Leseni na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoелеkezwa hapo juu.
- v. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).
- vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Mamlaka husika.
- viii. Uwasilishaji wa Taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria
- ix. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 12 Oktoba, 2023 saa 9.30 alasiri.
- x. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika Tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.
- xi. Maombi yote yawasilishwe kwa Barua kwenye anuani ifuatayo:

Mkurugenzi wa Mji,  
Halmashauri ya Mji Nanyamba,  
S.L.P 1490,  
NANYAMBA-MTWARA.

  
Thomas E. Mwalifu  
MKURUGENZI WA MJI

